HOTUBA YA UFUNGUZI MKUTANO MKUU WA TDC GLOBAL:

Ndugu Mgeni Rasmi,
Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ngugu Job Ndugai, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Zanzibar Mh Salum Maulid Salum, Balozi wa Tanzania katika nchi za Nordic,Baltic na Ukraine Dr. Wilbrod Slaa, Balozi Anisa Mbega Mkurugenzi wa dawati la Diaspora, mabibi na mabwana, wageni waalikwa na wanadiaspora kwa ujumla.
Naomba nianze kwa kumshukuru Mola kwa yote ambayo ametuwezesha kuyafanya ikiwemo kukutana katika mkusanyiko huu wa kipekee na kihistoria. Karibuni nchini Sweden. Pamoja na nyie mlioko katika ukumbi huu wako wajumbe wengine wengi wanashiriki Mkutano huu kwa njia ya Skype. Kwa wote karibuni na Asalaam Aleikhum. Tumsifu Yesu Kristo.Bwana Yesu asifiwe.
Naamini kwa wengi wenu, hii ni mara ya kwanza kufika nchini Sweden. Nawakaribisha sana. Kwa Ki-Swedish tunasema, “välkommen till Sverige”.
Ndugu zangu,
Niliyesimama mbele yenu ni Norman Jasson, Mwenyekiti wa muda wa Tanzania Global Diaspora Council au Baraza La Watanzania Diaspora Duniani au kwa kifupi TDC Global.
Kabla sijaendelea mbele sana, naomba kutoa shukrani za kipekee kwa ninyi nyote mlioitikia wito huu. Wengi wenu mmesafiri kutoka mbali. Mmeweka pembeni muda na shughuli zenu ili kujumuika hapa. Wako wengi wana;shiriki Mkutano huu kwa njia ya Skype na mitandao mingineyo ya kijamii wakati katika nchi wanazoishi ikiwa ni usiku mnono lakini wao wako macho kushiriki mkutano huu muhimu katika historia ya umoja wetu.
Mmefanya hivyo kwa imani kubwa mliyonayo kuhusu hiki tunachokizindua hivi punde. Isitoshe, shughuli ni watu. Na watu ndio sisi. Asanteni sana.
Pia naomba nitoe shukrani za kipekee kwa watu wote waliokesha usiku na mchana ili kufanikisha shughuli hii. Haikuwa kazi nyepesi.
Tunachokishuhudia hivi leo ni mchakato ambao ulianza rasmi tarehe 1 Novemba mwaka 2016. Kwa mapenzi na utashi wao, ndugu zetu **Hassan Ng’anzo (Norway), Jeff Msangi (Canada)** na **Abraham Sangiwa (UK)** waliulizana hivi kwanini watanzania tunaoishi nje ya nchi tusiwe na chombo cha kutuunganisha wote duniani?
Kilichofuata baada ya hapo ni mlolongo mrefu wa majadiliano na kutanua wigo kuwafikia watanzania. Hatua hiyo ilipelekes kuanzishwa uundwaji wa Kamati Ya Utendaji ya muda iliyokuwa na lengo la kuwafikia watanzania wengi zaidi kutoka katika nchi mbalimbali ulimwenguni.
Tunatoa shukurani za pekee kwa waasisi, wawakilishi wa Vyama vya watanzania kutoka visiwani na bara, vilivyopo Ughaibuni, kama vile DICOTA, umoja wa vyama vya watanzania Sweden TANRIKS, bila kumsahau Dada Rosemary C Jairo.

TDC Global pia inatoa shukran za dhati kwa uongozi mzima wa umoja wa watanzania Sweden TANRIKS kwa kukubali kuipokea TDC Global na kusimamia zoezi zima la usajili na majukumu yote katika kufanikisha umoja wa wanadiaspora wa Dunia nzima. Tunawatambua kwa namna ya pekee mbunifu wa jina TDC GLOBAL Dr Alex Pauline (UK); Dr Casta Tungaraza (Australia) ambae kwa kuzingatia weledi wake katika maswala ya sheria alifanikisha TDC Global kupata Katiba ambayo ndio inatumika kwa sasa.
Waswahili tuna msemo wetu unaosema,”Penye wengi, haliharibiki neno”. Lakini palipo na wengi na kila mmoja akiwa na hulka, maono na weledi tofauti, bila shaka pana mambo mengi. Kwa kifupi tu naomba niseme kwamba, mpaka kufikia hapa, TDC Global imepitia hatua nyingi na changamoto nyingi. Historia tunayoishuhudia leo, haikujengwa kirahisi. Tuna wengi wa kuwashukuru na kuwatunuku. Hatuwezi kuwataja wote hapa lakini shukrani ziwafikie wote kwa furaha ya pamoja.
Aidha, maadam tumefikia hapa, naomba tuseme kwa pamoja, **“YALIYOPITA SI NDWELE, TUGANGE YAJAYO”.** Tudhamirie kujenga, kuliko kubomoa. Tuweke mbele upendo zaidi ya chuki. Tukumbushane wajibu bila kuwekeana kinyongo. Tukumbushane tena na tena kwamba Umoja Ni Nguvu, Utengano Ni Udhaifu.

Ndugu mgeni rasmi, watanzania wenzangu,
TDC Global imesajiliwa rasmi hapa nchini Sweden mnamo tarehe 18 May 2018. Mpaka sasa TDC Global inafanya shughuli zake kutokea hapa nchini Sweden kwa kushirikiana na serikali kwa kupitia Ubalozi wake uliopo hapa Sweden chini ya Mh Balozi Dr. Wilbroad Slaa ambaye anaiwakilisha nchi na kumwakilisha Rais wa Serikali ya jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. John Pombe Magufuli.

TDC Global ilianzishwa ikiwa na malengo makuu yafuatayo;

•Kuhamasisha, kuunganisha na kuwawezesha watanzania waishio ughaibuni kwa kuandaa fursa ughaibuni ya kuwasiliana na serikali ya Tanzania na si kinyume chake.

Ili kufanikisha lengo au malengo haya na kwa uzingatia maslahi ya wanachama wake, baraza litafanya jitihada zifuatazo;

I.) Kushirikiana na watanzania wote wanaoishi ughaibuni na kukusanya maoni yao juu ya sera na sheria zinazoathiri ushiriki na mchango wao kamili kwa maendeleo ya Tanzania.

II.) Kushawishi serikali ya Tanzania kwa niaba ya wanachama wake wote
kuhusiana na masuala yote yenye maslahi kwao kiuchumi, kijamii na kitamaduni ikiwa ni pamoja na kupata faida zao kama wazawa wa Tanzania kama kuruhusiwa kuwa na "Hadhi Maalimu"(Special Status).

III.) Kutumia rasilimali watu na nyenzo za watanzania waishio ughaibuni katika kuendeleza maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ya Tanzania

IV.) Kujenga na kuitangaza picha nzuri ya Tanzania duniani kwa lengo la
kuongeza kiwango cha utalii na kufanya Tanzania kuwa chaguo la kwanza
katika biashara za kimataifa na uwekezaji Afrika.

b) kukuza, kutetea na kulinda haki ya uzawa na maslahi ya kibiashara ya Tanzania, na wajumbe wake, na hadi sasa inaweza kuwa sawa na malengo yafuatayo:

I.) Kusaidia na kuhamasisha maendeleo ya biashara na uwekezaji kati ya nchi ambazo watanzania walio ughaibuni na waliopo Tanzania.

II.) Kukusanya, kupata, kuchapisha na kusambaza taarifa na takwimu na maelezo mengine kuhusu mchango wa watanzania waishio ughaibuni katika biashara, uwekezaji, elimu, afya na mambo yanayohusiana nayo ambayo inaweza kuwa ya maslahi kwa wanachama wake na maendeleo ya Tanzania.

III.) Kuandaa Kongamano la kimataifa la watanzania waishio ughaibuni kila
Mwaka (kama hili) kuwezesha mazungumzo, kufuatailia maendeleo na malengo ya kitaifa , kuendeleza mipango ya utekelezaji na kujumuika na watu tofauti kutoka sehemu tofauti za dunia.

IV.) Kukuza mahusiano ya kijamii na kiuchumi kati ya wanachama wa Diaspora duniani kote na watu maarufu wenye nyadhifa tofauti kutoka Tanzania kwa maslahi husika ya wanachama wote kwqa ujumla.

V.) Kushirikiana au kuwa na uhusiano na kuchangia shughuli za taasisi, jamii, vyama au kampuni zinazofuata malengo yanayofanana ambayo yanaweza kuwa ya faida kwa wanachama.

c.) Kuchangia kwenye jitihada za wanachama ili kuboresha ubora wa maisha ya mtu binafsi, ulinzi wa maslahi yao, mahusiano na ushirikiano.

d.) Kuwezesha kuundwa kwa nafasi mpya za ajira na fursa za mafunzo Tanzania kwa kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha wanachama wake kushiriki katika uwekezaji, biashara, utalii, kupeana ujuzi na kuongezeka utumiaji wa fedha za kigeni nchini

e.) Kuhamasisha wanachama kuunda mfuko wa hiari wa baraza ambao utasaidia kuchangia katika elimu, afya, huduma za ulemavu, makazi na uwepo wa chakula.

f.) Kuandaa shughuli za kuchangia mfuko kutoka kwa vyama vyenye nia katika ngazi ya kitaifa na kimataifa ili kutimiza malengo ya shirika.

g.) Kuimarisha roho ya kujitolea kwa kuwa na watanzania waishio ughaibuni wanaojitolea wakiwa na mpango kazi wa muda mfupi na wa muda mrefu ili kuratibu watanzania waishio ughaibuni kushiriki katika shughuli za dharura au utoaji wa misaada kama itakavyohitajika.

h.) Kukusanya na kusambaza habari, kuelimisha na kuwajulisha juu ya mambo yote yanayoathiri madhumuni ya watanzania waishio ughaibuni kupitia makusanyiko, semina, warsha, mikutano na njia nyingine za utangazaji ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari.

i.) Kufanya chochote au vitu vyote vinavyofaa ili kufikia malengo yaliyotajwa awali.

j.) Kuungana na mashirika binafsi, ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali kwa niaba ya wanachama katika kufikia malengo ya TDC Global.

k.) Kuwapa wanachama habari kuhusu sera, taratibu zinazohusiana na fursa za uwekezaji nchini Tanzania, kuwezesha ushiriki wa wanachama katika michakato ya zabuni na kuunga mkono miradi nchini Tanzania.

Kutoa huduma za ushauri za zabuni na maendeleo ya biashara kwa wanachama kama inavyohitajika na kuwa mwakilishi kwa wale wanaotaka kuidhinisha baraza kushughulikia biashara kwa niaba yao.

l.) Kuandaa maonyesho ya biashara pamoja na matukio ya kijamii na kiutamaduni kusaidia kazi ya baraza na hatimaye kukuza picha nzuri ya Tanzania na watanzania popote walipo

Ndugu mgeni rasmi, wageni na watanzania wenzangu

Malengo ya baraza na watanzania waishio nje ya nchi yaani Diaspora ni mengi. Yanahitaji ushirikiano na zaidi yanahitaji upendo wa dhati kwa nchi yetu Tanzania, watanzania wenzetu na bila shaka serikali yetu.

Nafurahi kusema kwamba malengo haya yote yaliandaliwa kwa kuzingatia jambo moja muhimu; upendo na uzalendo kwa nchi yetu, ndugu, jamaa na marafiki zetu hususani waliopo nyumbani.

Ili kufanikisha malengo niliyoyataja hapo juu, lazima tufanye kitu ambacho vizazi vilivyopita havikuwahi kufanya au hata vilipojaribu, havikufanikiwa ipasavyo. Mojawapo ya mambo hayo ni kuamua kuonyesha njia kwa vitendo. Maneno yetu yaendane na kulingana na vitendo vyetu.

Mkusanyiko huu, ndugu mgeni rasmi, ni ishara kutoka kwetu kwamba sasa tumeamua kuendeleza masuala yetu kwa vitendo zaidi ya maneno. Kielelezo sahihi cha Matendo na kuwa TDC Global kwa sasa imekamalisha usajili katika Kamati ya Biashara na Uchumi Chamber of Commerce itakayosimamiwa na TDC Global yenyewe, na Chambers zingine zitakazo sajiliwa na wanachama wetu mbalimbali, Chambers zitakuwa milango muhimu ya kushawishi na kichocheo kikubwa cha kukuza Uchumi wa Taifa na mama yetu Tanzania.

Pamoja na nia yetu nzuri, tunatambua na kuheshimu kwamba Tanzania ni nchi inayoongozwa kwa kuzingatia utawala wa sheria na kidemokrasia. Kwa kuzingatia hilo, naomba kuchukua fursa hii kuwakilisha ombi la msingi ambalo naamini ni kutoka kwa diaspora wengi; tunaiomba serikali ilitizame kwa jicho la pili suala la hadhi maalumu (special status). Pia tunaiombe Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki kuongeza Kazi ya kuandaa Sera ya Diaspora ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itasaidia Wana diaspora kuchangia maendeleo ya nchi kwa Kasi zaidi.

Faida na fursa zinazoweza kutokana na kurasimisha masuala haya ni nyingi. Nisingependa kuchukua muda hapa kuzielezea. Takwimu zipo. Tafiti zipo. Tunaamini kwamba serikali yetu sikivu, imesikia, imeona na inaendelea kusikia na kuona. Ili tufanikiwe zaidi tunaamini kwamba lazima tufanye hivyo kama Tanzania moja!

TDC Global ina imani kubwa na serikali yetu. Tunaona na kuthamini kasi ya utendaji na uwajibikaji uliyopo. Matunda na matokeo yanaonekana. Ni imani yetu kwamba serikali italipa ombi la Wanadiaspora la Hadhi Maalum (Special Status) litapewa umuhimu wa kipekee. .

Kwa miaka mingi, hili limekuwa ombi kubwa kutoka kwa diaspora. Tunaamini kwamba chini ya uongozi wa Rais Dr. John Pombe Magufuli, hatua stahiki zitachukuliwa na maombi yetu yatafanyiwa kazi ili Wanadiaspora waweze kutoa mchango wao stahiki kwa maendeleo ya Mama yetu Tanzania. Ni imani yetu kuwa mchakato wa Sera ya Diaspora unaoendelea utapewa pia kipaumbele ili dhamira ya Lengo hili kubwa la Wanadiaspora liweze kubebwa na Sera na Sheria za Taifa letu.Kwani akiahidi jambo Wanadiaspora tumesikia sauti ya tarumbeta. Tupo tayari kuitikia wito kwa nguvu mpya na kasi mpya.

Naomba nimalizie kwa kusema kwamba,diaspora tupo tayari na imara kushirikiana na serikali na wananchi wenzetu, ndugu, jamaa na marafiki katika kujenga Tanzania iliyo bora kwa kizazi cha sasa na kijacho. Tunaamini katika kuwajibika sio tu kwa serikali bali pia familia zetu, jamii zetu na nchi yetu. Wanadiaspora tunaiishi kauli ya " Hapa Kazi Tu" kwa vitendo, kwani bila kazi hata hapa ughaibuni hakuna kula bila kazi.

Asanteni kwa kunisikiliza. Mwenyezi Mungu awabariki. Mungu ibariki Tanzania.

''PAMOJA TWAWEZA – MTU KWAO NDIO NGAO''

Norman Jasson
Mwenyekiti
TDC Global